


Haaaa! Nyumbani
kwetu, kuna
ng'ombe wa ajabu.




Ana pembe moja
tu na hana mkia.

Ni ng'ombe mzuri
sana.



Ni ng'ombe mnono
aliye na tumbo
kubwa.




Ni ng'ombe aliye
na nguvu.



Mchungaji
anampenda
ng'ombe huyu
sana.

Amemfunza
kuitambua sauti
yake pekee.




Anapokuwa
malishoni,
ng'ombe huyu
hujitenga na
ng'ombe wengine.



Ni ng'ombe aliye
hodari katika vita.

Ng'ombe wengine
wanamwogopa.



Watu wengi
wanamjua
ng'ombe huyu.
Wanamwogopa
kwa sababu yeye
hupigana kwa
pembe yake moja.

Ukikutana na
ng'ombe wa aina
hii, utafanyaje?